

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIAOFISI YA**

MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE, WILAYA YA HAI.



TANGAZO LA KUPATA WAZABUNI WA VIFAA VYA UJENZI

('LOCAL MATERIALS SUPPLIERS')

UJENZI WA CHUO CHA UFUNDI STADI CHA WILAYA YA HAI.

TAREHE YA TANGAZO : 20.04.2023. "TANGAZO LIMERUDIWA"

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kujenga Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) katika Wilaya ambazo hazina Vyuo ikiwepo wilaya ya Hai.

Ujenzi huu unategemea kutekelezwa kwa utaratibu wa 'Force Account' ambapo Wizara inategemea kutumia taasisi zake ambazo ni; Ofisi za Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule, Vyuo vya Ualimu (TCs) na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) kama watekelezaji na Chuo Kikuu cha Ardhi (Ardhi University) kama Mshauri Elekezi wa Mradi.

Aidha, ili kutekeleza mradi kwa utaratibu wa 'Force Account' watekelezaji wanatakiwa kununua vifaa vya ujenzi ambavyo vitatumika na fundi Mkuu kwa majengo yanayotegemewa kujengwa. Baadhi ya vifaa vya ujenzi (Materials from Local Suppliers) vinavyohitajika ni kama inavyooneshwaa katika jedwari hapa chini.

Jedwali: Baadhi ya vifaa vya ujenzi (Major Local Materials) vinavyohitajika.

Na.	Vifaa vya ujenzi vinavyohitajika	Maelezo
1	Matofali	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi
2	Kokoto	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi
3	Mawe	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi
4	Mchanga	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi
5	Kifusi	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi
6	Vifaa vya dari (gypsum boards etc)	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi

7	Milango	Mzabuni atatakiwa kupachika katika majengo
8	Madirisha	Mzabuni atatakiwa kupachika katika majengo
9	'Tiles'	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi
10	Vifaa vya umeme na bomba	Mzabuni atatakiwa kupeleka hadi eneo la ujenzi

Hivyo, Mthibiti Mkuu ubora wa Shule Wilaya ya Hai kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST)_anawatangazia wazabuni wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu kuomba kazi kama ilivyoelezwa hapa chini:

Sifa na masharti kwa wazabuni wanaohitajika.

- 1) Mzabuni lazima awe amesajiliwa kufanya biashara ya bidhaa zilizotajwa katika tangazo hili, na awasilishe nyaraka zifuatizo:
 - a) Nakala ya Leseni ya Biashara.
 - b) Cheti cha Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN).
 - c) Cheti cha usajili wa' BRELA'.
 - d) Barua inayooonesha kwamba bei ya vifaa vya ujenzi alivyojaza hazitabalika kwa muda wa miezi sita (06).
 - e) Barua ya maombi ikitaja vifaa vya ujenzi anazoomba.
 - f) Wasifu wa kampuni (Company Profile).
- 2) Mzabuni atalipwa malipo yake baada ya kuleta vifaa vya ujenzi alivyoshinda (Post-paid).
- 3) Mzabuni lazima awe na mashine ya ki-eletroniki ya kutolea risiti (EFD Machine) na awasilishe nakala ya uthibitisho wa mashine hiyo.
- 4) Mzabuni lazima awasilishe nakala ya kitambulisho cha benki cha kampuni husika.
- 5) Uchambuzi wa wazabuni (Evaluation) utafanyika kulingana na bei halisi ya soko kwa kila 'materials' au kifaa kinachohitajika katika mradi, na siyo ujumla wa hati msako (quotation).
- 6) Mzabuni atakayeshinda kuleta 'materials'za ujenzi/vifaa lazima asaini mkataba/makubaliano kabla ya kuleta vifaa vya ujenzi alivyoshinda.
- 7) Mwombaji atatakiwa kudurufu (photocopy) nakala ya hati msako (Quotation) kwa gharama zake mwenyewe ili kujaza, kufunga kwa lakiri (sealed) na kuwasilisha nakala halisi (original) moja na nakala vivuli (copies) mbili.
- 8) Inasisitizwa kuwa mzabuni lazima ajaze bei ya vifaa vya ujenzi na kubainisha gharama za usafiri hadi eneo la ujenzi na malipo yatafanyika baada ya vifaa hivyo kupokelewa katika eneo la ujenzi husika. Aidha ni lazima mzabuni ajaze vipengele vyote vya loti alizochagua.

- 9) Maombi ya zabuni yawasilishwe kwa njia ya mkono ofisi za masijala ya wazi (Registry Office) ya Ofisi ya Mthibiti Ubora wa Shule, Wilaya ya Hai. yakiwa yameandikwa kwa herufi kubwa:

MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE
OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE, WILAYA YA HAI
MRADI WA UJENZI CHUO CHA UFUNDI STADI CHA WILAYA
S. L. P. 11-HAI.

- 10) *Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 28.04.2023 siku ya Ijumaa saa 5:00 Asubuhi na ndiyo siku ya ufunguzi.*
11) Kwa maelezo zaidi wasiliana kwa namba: 0754855699

Tangazo hili Limetolewa na:

A. Kawau **MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE (W)**
WILAYA YA HAI
ASTERIA V. KAWAU
MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE

OFISI YA MTHIBITI MKUU UBORA WA SHULE, WILAYA YA HAI.

KNY: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia